# Mbwa ni fedha inayobweka

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. Na. 13, Alhamisi Januari 30, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100

**AZIMIO LA DAR...**

# Sura halisi ya Dk. Samia hii hapa



- Ajipambanua kutanguliza mbele maslahi ya taifa
- Sasa azipambania kaya Milioni 8.3 ili zipate umeme wa uhakika
- Katika kaya hizi kuna wajasirimali wengi wanaopambana 'kutoboa'

" Ukiondoa nishati ya umeme inayotegemewa na wajasiriamali wengi, Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha mabilioni ya mikopo kwa wanufaika zaidi ya milioni 1.7 ambao wapo katika sekta za kilimo, mifugo... uk.2

# Ajira sekta ya umma ni mchakamchaka




## Unataka kuanzisha biashara huna senti?

# Sura halisi ya Dk. Samia hii hapa

NA MWANDISHI MAALUM

**NI MTU WA WATU! Picha halisi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kupigania maslahi ya Watanzania inazidi kujionyesha, kutokana na mipango na mikakati iliyowekwa na serikali yake katika kipindi hiki alichopo madarakani.**

Moja, wakati ikifahamika wazi umuhimu wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya watu, Dkt. Samia ameithibitishia dunia kuhusu Tanzania kuunganisha umeme kwa kaya milioni 8.3 zaidi ifikapo mwaka 2030.

Kupitia mpango mahususi wa kitaifa wa umeme kwa nchi za Afrika, Tanzania itahitaji Sh trilioni 33 na kuongeza kasi kuunganisha umeme nchini hadi kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

Mpango huo utawezesha Serikali kukamilisha usambazaji umeme katika Vitongoji vyote 64,359 nchini ifikapo 2030 na utapandisha kiwango cha uunganishaji wa umeme kutoka asilimia 46 ya sasa hadi kufikia asilimia 75.

Rais Dkt. Samia ambaye amekuwa kinara wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ameweka bayana kuwa mpango huo wa Nishati pia utasaidia kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, ikiwemo gesi asilia na majiko banifu.

Upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwan a ipo kwenye asilimia zaidi ya 78, huku uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1470 hadi megawati takriban 3,077 na vijiji vyote 12,318 ambapoo baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji ambapo katika vitongoji 64,000 nchini, vitongoji takriban 36,000 vimepelekewa umeme.

Ukiondoa nishati ya umeme inayotegemewa na wajasiriamali wengi, Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha mabilioni ya mikopo kwa wanufaika zaidi ya milioni 1.7 ambao wapo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwasaidia kujikwamua kutoka pale walipo.

Dkt. Samia pia amefanikiwa kutoa mikopo isiyo na riba ya Sh bilioni 240.9 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana 164,443 waliomaliza taasisi za elimu ya juu na kati.

Pia kiwango cha ukuaji wa pato la taifa kimekuwa kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.1 mwaka 2023.

Katika kujenga Tanzania imara, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha utekelezaji wa miradi 17,421 ya sekta za afya na elimu na kutoa ajira za muda kwa maelfu ya Watanzania. Ajira za muda ni kwa kaya za walengwa 662,374 Tanzania Bara na Visiwani.

Kingine ni kiwango cha ukuaji wa uchumi kilikadiriwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na serikali imedhibiti mfumuko wa bei hadi asilimia 3 mwaka 2024 kutoka asilimia 3.1 mwaka 2020.

Mapato ya ndani yaliongezeka kufikia Sh trilioni 13.54 mwaka 2024 kutoka Sh trilioni 8.1 mwaka 2020. Idadi ya walipa kodi iliongezeka hadi milioni 6.4, na serikali imeondoa kodi zisizo na tija ili kuchochea maendeleo.

Haya ni machache tu, kati ya mengi ambayo yanaonyesha Rais Dkt. Samia anavyoipambania kwa nguvu zote Tanzania ili wananchi wake wawe na maisha bora zaidi.

# Ruvuma miradi ya maji yakaguliwa

NA ALBANO MIDELO, Songea

**MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas, amefanya ukaguzi wa maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Miji 28 katika Mji wa Songea.**

Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 145.77 na unalenga kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa eneo hilo.

Kanali Abbas ametoa wito kwa mkandarasi kuhakikisha kazi inaendelea bila kusimama.

Amehimiza kutumia vyanzo vingine vya fedha ili kuhakikisha ujenzi unasonga mbele kwa ufanisi.

"Mkandarasi anapaswa kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa haraka,ni muhimu mradi huu ukamilike kwa ubora na ufanisi wa hali ya juu," alisema Kanali Abbas

Akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo, Mhandisi Vicent Bahemana kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) amesema kuwa ujenzi huo unahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka Mto Njuga, uliopo kijiji cha Kikunja katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Amesema mradi huo unatarajia kuongeza uzalishaji wa maji hadi lita milioni 17 kwa siku, hatua hali ambayo itasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika mji wa Songea.

Mkurugenzi wa SOUWASA Mhandisi Patrick Kibasa amesema mradi huo huo unajumuisha ujenzi wa matenki matatu yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 9 za maji pamoja na usambazaji wa bomba za maji umbali wa kilomita 34.7.

Mradi wa Miji 28 unatekelezwa na kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC). Hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia tano.



# Chanjo ya mifugo lazima

NA MWANDISHI WETU

**KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe amewataka wazabuni waliopewa jukumu la kusambaza chanjo kwa ajili ya kampeni ya chanjo ya mifugo nchini kuhakwikisha kazi hiyo wanaifanya vyema kwa kushirikiana na wazalishaji.**

Ameyasema hayo wakati wa Hafla Fupi ya Utiaji Saini Mikataba baina ya Wizara na Wazabuni hao watakaosambaza Chanjo ya Mifugo Nchini iliyofanyika jijini Dodoma.

Prof. Shemdoe ameongeza kuwa utoaji wa chanjo hiyo kwa mifugo inatakaiwa kufanyika chini ya uangalizi wa wazalishaji kwa kushirikiana na wataalamu watakao kuwa wanafanya kazi hiyo ili kusaidia kutatua changamoto zitakazojitokeza wakati wa zoezi hilo.


Aidha Prof. Shemdoe ametoa shukrani kwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia na kuwezesha utowaji wa chanjo hiyo mwaka huu na kuwapa kipaumbele makampuni yanayozalisha chanjo ndani ya nchi kuweza kusambaza chanjo hiyo nchi nzima.

Kampuni zitakazotumika katika uzalishaji wa chanjo wa chanjo hiyo ni pamoja na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Hester Biosciences Afica Limited (HBAL) na Novel Vaccine and Biological Limited (NOVABI).



# Mwinyi: Vyuo vikuu vijikite katika tafiti

NA MWANDISHI WETU, Z'bar



**RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk, Hussein Ali Mwinyi amevikumbusha vyuo vikuu viliyopo nchini umuhimu wa kujikita katika kufanya tafiti ambazo zitatoa ufunbuzi wa changamoto za kijamii na kuzisambaza kwa watumiaji.**

Rais Dk. Mwinyi ametoa tamko hilo hivi karibuni katika mahafali ya 24 ya Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al Sumait Chukwani Wilaya ya Magahribi B, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Dk. Mwinyi alitoa wito kwa viongozi wa vyuo vikuu kuendelea kujenga uwezo wa kufanya tafiti kwa wafanyakazi kwa kutumia fursa zilzopo pamoja na kushirikiana na vyuov vikuu vingine vyenye wataalamu waliobobea katika tafiti kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wazalendo.

Aidha, amesisitiza umuhimu wa kusamabaza matokeo ya tafiti kwa watumiaji kwani bila ya kuasambaza kwa watumiaji ni kupoteza rasilimali.

Rais Dk. Mwinyi amefahamisha kuwa kutosambazwa kwa tafiti kunapunguza hadhi za vyuo vikuu kama vitovu vya kuleta mabadiliko ya kijamii na kutoa rai kwa vyuo vikuu kuandaa mpango maalum Utakaohakikisha Matokeo ya Tafiti yanawafikia watumiaji.

Rais Dk. Mwinyi ameeleza kuwa ni muhimu kwa wizara na idara za Serikali kushirikiana na vyuo vikuu kufanya tafiti na kutumia Tafiti mbalimbali kuleta maendeleo katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

# Kilimo kufuatilia athari za viuatilifu

NA MWANDISHI WETU

**KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo Gerald Mweli amesema Wizara ya Kilimo itashirikiana na wadau mbalimbali kama Wizara ya Afya, Jeshi la Polisi, Taasisi na Mashirika mbalimbali katika kutatua changamoto zinazotokana na athari za viuatilifu vinavyotumika katika shughuli za kilimo.**

Katibu Mkuu Mweli ameshiriki kama mgeni rasmi katika Kikao cha Wadau wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) kujadili matukio na madhara ya sumu za viuatilifu yaliyotokea nchini katika mwaka 2017-2024 kilichofanyika juzi, mkoani Dodoma.

Amesema kuwa miongoni mwa malengo ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2030 ni kuongeza uelewa wa matumizi sahihi ya viuatilifu kuanzia katika ngazi ya manunuzi, uhifadhi pamoja na matumizi.

Mweli ameeleza zaidi kuwa Wizara ya Kilimo itaendelea na tafiti za kugundua viuatilifu bora zaidi na kuhakikisha wauzaji wa maduka ya pembejeo wanakua na elimu ya kutosha katika kutoa ushauri kwa wakulima ili kukabiliana na changamoto za kilimo pamoja na kuzingatia matumizi sahihi ya viuatilifu.

# Uhamiaji watakiwa kusaka wahamiaji haramu

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa amemuagiza Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji CGI Dkt. Anna Makakala kuendelea na operesheni, misako na doria za kukamata wahamiaji haramu na kuhakikisha wageni wote wanaoingia ndani ya nchi, wanafuata taratibu na sheria za kuingia nchini.**

Bashungwa ameelekeza hayo wakati hivi karibuni alipofanya ziara Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji, Dodoma ambapo amesema Serikali haitakuwa na muhali na mtu yeyote ambaye anaingia nchini bila kufuata Utaratibu na Sheria za Nchi yetu.

Bashungwa amemuelekeza pia na Dkt. Anna Makakala kuhakikisha kila Ofisi ya Wilaya ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inakuwa na Afisa wa Uhamiaji ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Nitakapokuwa naenda kwenye wilaya, nikifika ofisi za NIDA nikute kuna Afisa wa NIDA lakini awepo Afisa wa Uhamiaji ambao wanashirikiana kuwahudumia Wanzania ili kuepuka usumbufu usio kuwa na tija kwa Wananchi kutoka ofisi moja kwenda ofisi nyingine," amesisitiza Bashungwa

Awali, Dkt. Anna Makakala ameeleza kuwa Idara ya Uhamiaji inaendelea na misako, doria na kaguzi mbalimbali kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarishwa.

"Katika mwaka 2024 tumefanya Operesheni, misako na doria nchi nzima, jumla ya Wahamiaji wa makosa mbalimbali 14,368 walikamatwa na kuchukuliwa hatua."

# Ajira sekta ya umma ni mchakamchaka

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amesema suala la ushindani katika upatikanaji wa ajira katika Utumishi wa Umma ni jambo lisiloepukika kutokana na idadi kubwa ya wasomi iliyopo kwa sasa**

Amesema dhamira hiyo ya kuhakikisha waombaji kazi wote wanafanya usaili kunasaidia kuwapata watumishi wenye sifa stahiki katika utumishi wa umma na kuondoa dhana ya upendeleo iliyokuwa imejengeka miongoni mwa jamii.

Simbachawene ametoa kauli hiyo alipotembelea kituo cha usaili wa kada ya ualimu Mkoani Singida ili kujionea mwenendo wa zoezi hilo, ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 inayoelekeza kuwa ajira katika utumishi wa umma zipatikane kwa ushindani

"Hakuna palipoandikwa kuwa watu wote waliosoma wataajiriwa na Serikali ndio maana ajira za serikali ni za ushindani kwani waliosoma ni wengi lakini nafasi ni chache."

Amesema Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma mara baada ya kutangaza kazi za ualimu, waombaji 201,707 walijitokeza kuomba lakini baada ya mchujo kutokana na baadhi kutokukidhi vigezo ikiwemo kutokuweka baadhi ya vyeti kama ilivyoelekezwa walichujwa hadi kufikia waombaji 107,746.

.Simbachawene ametumia fursa hiyo kuwasihi waombaji kazi kuhakikisha wanaweka vyeti vyao vinavyotakiwa ili kuepuka mchujo katika hatua za awali.

Usaili wa kada ya ualimu unaendelea katika vituo mbalimbali nchi nzima na utakamilika Februari 24 Mwaka huu.

# Ubunifu watakiwa katika uzalishaji

NA MWANDISHI WETU

**NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sospeter Mtwale amewataka Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa wa Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji kuwa wabunifu katika kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ya kukuza uchumi inayolenga kutatua changamoto za uchumi na uzalishaji katika mikoa na halmashauri wanazozisimamia.**

Mtwale wito huo jijini Dodoma, wakati akifungua kikao kazi cha Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa wa Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji kilicholenga kujadili utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na kuandaa mipango ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

"Sehemu za uchumi na uzalishaji katika mikoa ndio zinabeba dira ya ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu katika nchi yetu hivyo ni muhimu mipango yenu ilenge vipaumbele vya Serikali kwa kuzingatia uendelezaji wa uchumi mahalia," Mtwale amesisitiza.

Mtwale amehimiza kuwa, katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea na maandalizi ya Mipango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ni vema mipango na bajeti za mikoa na halmashauri zikazingatia mwongozo wa bajeti na vipaumbele vya nchi ili kuakisi utatuzi wa matatizo ya kiuchumi yanayowakabili wananchi na taifa kwa ujumla.

Sanjari na hilo, amewakumbusha Makatibu Tawala hao Wasaidizi wa Mikoa kuwa, wanajukumu muhimu katika maendeleo ya taifa hivyo waendelee kutekeleza majukumu yako kwa weledi na uzito unaostahili ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao hususani katika kutatua changamoto za uchumi na uzalishaji kwenye mikoa na halmashauri wanazozisimamia.

Kwa upande wake, mwakilishi wa makatibu tawala hao wasaidizi Said Maditto ambaye ni Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya amesema kuwa kitendo cha kufanya kikao kazi na wakurugenzi wa wizara za kisekta ni fursa ya kujenga ushirikiano wa kiutendaji katika kutekeleza mikakati na mipango ya kukuza uchumi nchini.

Aidha, Maditto ameahidi kuwa watatekeleza kwa vitendo maelekezo yote aliyoyatoa pamoja na kutekeleza maazimio wakakayotokanayo katika kikao kazi hicho kwa lengo la kuandaa mikakati na mipango endelevu itakayokuza uchumi wa taifa.

Naye, Mkurugenzi wa Tawala za Mikoa Ofisi ya Rais-TAMISEMI Beatrice Kimoleta amesema TAMISEMI iliona ni muhimu kukutana na Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa wa Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji pamoja na wakurugenzi wa Wizara za Kisekta kwa ajili ya kupata maoni, maono na mtazamo wa namna bora ya kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ya kukuza uchumi nchini.

# Ofisi ya Rais-Utumishi wapewa angalizo

MWANDISHI WETU

**WATUMISHI wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wamesisitizwa kuzingatia Itifaki na Diplomasia katika utendaji kazi Ili kujenga heshima ya ofisi kwa manufaa ya nchi.**

Wito huo umetolewa na Balozi mstaafu Nelson Lyimo wakati akifanya wasilisho kuhusu Itifaki na Diplomasia kwa Watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.

Balozi Lyimo amesema, Ofisi ya Rais-UTUMISHI ni muhimu kwa Taifa la Tanzania kwa kuwa inasimamia rasilimaliwatu, hivyo Watumishi wake wanatakiwa kuzingatia Itifaki na Diplomasia wakati wote wanapotekeleza majukumu yao katika ofisi hiyo.

Amewasisitiza Watumishi kuwa wasikivu kwa wateja wanaowahudumia na kuona namna ya kuwasaidia kupata majibu au suluhisho la suala ambalo mteja husika ameliwasilisha.

"Niwaombe kila mtumishi wa ofisi hii ajipime namna anavyotoa huduma kwa wateja kwani ndio kipimo cha tabia njema wakati wa utendaji kazi, jambo ambalo litaenda kuitangaza ofisi vizuri kwa maslahi mapana ya taifa, amesisitiza Balozi Lyimo.

Akihitimisha mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi hao, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala, Musa Magufuli alimshukuru Balozi Lyimo kwa kutoa elimu hiyo kwa watumishi hao ambayo itaboresha utendaji kazi kwa watumishi wao.



## MAONI

# Hongera Rais Samia mkakati kaya Milioni 8.3 kupata umeme

**JUZI Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema kuwa Mpango Mahsusi wa Kitaifa kuhusu Nishati (National Energy Compact) uliozinduliwa unalenga kuiwezeseha Tanzania kuunganisha umeme kwa kaya milioni 8.3 zaidi ifikapo mwaka 2030.**

Rais Dkt. Samia aliyasema hayo wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika kuhusu Nishati uliofanyika kwa muda wa siku mbili katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere, Dar es Salaam na kumalizika juzi.

Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano huo uliohudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka Burundi, Botswana, Congo, Comoros, Djibouti, Ethiopia, Gabon, Ghana, Guinea Bissau, Kenya, Lesotho, Liberia, Libya, Madagascar, Malawi, Mauritania, Nigeria, Sierra Leone, Somalia na Zambia.

Vile vile, mkutano huo ulihudhuriwa na Wawakilishi wa Wakuu wa Nchi na Serikali, Wakuu wa Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, Mashirika ya Kimataifa, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa lengo la kuongeza kasi ya usambazaji umeme barani Afrika ili kuwaunganisha watu milioni 300 na umeme katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Rais Dkt. Samia alisema kuwa kwa kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa nishati ya umeme, mkutano huo ulioandaliwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika utawezesha kuleta mageuzi ya kiuchumi, kukua kwa viwanda, kupunguza umaskini na kuimarisha ustawi wa watu.

Mkutano huo ulifanikiwa kupata ahadi za ufadhili wa Dola za Marekani Bilioni 40 kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa umeme barani Afrika. Aidha, jumla ya nchi za Afrika 12 zimeingia kwenye Mipango Mahsusi wa Kitaifa kuhusu Nishati.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa kupitia Mpango Mahsusi kuhusu Nishati, Tanzania inakusudia kuvutia mitaji na uwekezaji zaidi itakayowezesha kuongeza uzalishaji wa umeme nchini na kukukamilisha kuunganisha Mtandao wa Umeme wa Tanzania na nchi jirani ili kuwezesha biashara ya kuuza na kununua nishati hiyo.

Mpango huo utawezesha Serikali kukamilisha usambazaji umeme katika Vitongoji vyote 64,359 nchini ifikapo 2030. Vilevile, Mpango huo utapandisha kiwango cha uunganishaji wa umeme kutoka 46% ya sasa hadi kufikia 75%.

Kwetu Rais Dkt. Samia ambaye amekuwa kinara wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, alifurahisha wengi kwa kuweka bayana kuwa mpango huo wa nishati pia utasaidia kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, ikiwemo gesi asilia na majiko banifu.

Kila la kheri Rais Dkt. Samia katika mpango mkakati huo na tunaamini kwa dhati kabisa utafanikiwa katika hili, sisi tutaendelea kukuunga mkono ili utimize hili kwa Watanzania.




## FIKRA YA MJASIRIAMALI

# Azimio la Dar ukombozi kwa 'mchumia tumbo'

MWIGI MWIGASI
0784 03 03 51

**MWANZONI mwa wiki kulikuwa na mkutano wa siku mbili kujadili mustakabali wa umeme ndani ya Bara la Afrika, ambapo ulishirikisha wakuu wa nchi zilizomo ndani ya bara hili, pamoja na wakuu wa taasisi mbalimbali za kimataifa.**

Tunasema Afrika imejikomboa yenyewe kuhusu suala la nishati, baada ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika Kuhusu Nishati kuhitimishwa, huku wakuu waliohudhuria wakitia saini 'Azimio la Dar' litakalowezesha Waafrika milioni 300 kufikishiwa huduma ya umeme ifikapo mwaka 2030.

Mkutano wa wakuu wa nchi na viongozi wengine a vyombo vya fedha, ulimalizika lakini kabla ya hapo ulitanguliwa na mawaziri wa kisekta kabla ya viongozi hao kuhitimisha mkutano huo.

Tulimsikia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akisema Tanzania ni moja kati ya nchi 12 zitakazozindua mpango mahususi wa kitaifa kuhusu nishati. Kupitia mpango huo unatarajiwa kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini hadi kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

Fahamu akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dkt. Samia alivunja na kuandika rekodi ya aina yake kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Nchi ambao wakuu wake walishiriki ni Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Mbali na hilo, Afrika imeelezwa kupiga hatua katika suala zima la upatikanaji nishati ya umeme toka nyingi kati ya hizo zipte uhuru miaka ya 1960.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko alisema hayo jana kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika 'Mission 300' uliokuwa unafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

"Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571.kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

"Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160."

Kwangu nishati ni kila kitu kwani inakwenda kumkomboa mjasiriamali ambaye anapambana, ili tu awe na maisha bora na hilo linatimia kutimiza ndoto za wengi kutaka kuwa na maisha yanayofanana na utu wa binadamu.

Mjasiriamali yoyote atakaa na kufurahi azimio lililopitishwa, sasa ni mwanzo wa kuitoa Afrika katika giza lililo kuu.

# Unataka kuanzisha biashara, huna hata senti

NA MWANDISHI MAALUM

**KIKWAZO cha wengi kuingia kwenye biashara kimekuwa ni mtaji, hiki kimekuwa kilio cha kila anayetaka kuingia kwenye biashara na akashindwa au aliye kwenye biashara na kushindwa kuikuza.**

Kila anayeshindwa kuingia kwenye biashara au aliye kwenye biashara na kushindwa kuikuza, sababu yake kuu huwa ni kukosa mtaji.

Lakini mimi nimekuwa nawaeleza watu ukweli huu, kukosa mtaji hakujawahi kumzuia mtu mwenye nia ya kweli kuingia kwenye biashara. Bali kukosa mtaji ni sababu rahisi kwa yeyote kutumia, ambayo hakuna anaweza kukukatalia.

Naamini bila ya shaka yoyote kwamba mtu yeyote anaweza kuanzisha na kukuza biashara yake hata kama hana kabisa mtaji wa kuanzisha biashara hiyo.

Nina ushahidi kwangu binafsi na ushahidi kutoka kwa wengine wa jinsi gani hilo linawezekana na leo nakupa nafasi ya wewe kujua hili, ili uache kutoa visingizio na uanzishe au kukuza biashara yako.

**AINA ZA MITAJI**

Watu wengi wanapozungumzia mtaji wa biashara, huwa wanazungumzia aina moja tu ya mtaji, ambayo ni mtaji fedha. Wakikosa aina hii ya mtaji, wanaona hawawezi kuingia kwenye biashara.

Usichojua ni kwamba kuna aina tano za mtaji wa kuanzisha biashara, fedha ni moja ya aina hizo, ila kuna aina nyingine 4 ambazo ukijua jinsi ya kuzitumia vizuri utaweza kuanzisha biashara.

Ninachotaka kukuambia hapa ni kwamba, hata kama huna fedha, kuna aina nyingine za mtaji unazo katika hizo tano, hivyo usikate tamaa na kujiambia kwa kuwa huna mtaji basi huwezi kuingia kwenye biashara.

**VYANZO VYA MTAJI FEDHA**

Inapokuja kwenye mtaji fedha, wengi wanaokwama kupata mtaji huu huwa wanahangaika na njia moja tu, na wengi ni njia ya mkopo. Utawasikia wengi wakisema sina sifa ya kukopesheka, hivyo siwezi kupata mtaji wa kuanza biashara.

Hili pia siyo sahihi, kwa sababu vyanzo vya mtaji wa fedha siyo mkopo pekee.

Kuna vyanzo vikubwa vitano vya kupata mtaji wa fedha kwenye biashara, mkopo ni moja kati ya njia hizo tano na ambao una vikwazo vingi.

Kuna vyanzo vingine vya kupata mtaji fedha, tena ambavyo ni rahisi na visivyokuumiza kama kilivyo chanzo cha mkopo. Ulivijua vyanzo hivyo na jinsi ya kuvitumia vizuri, utaweza

Huwa wanasema pesa huleta pesa lakini wakati mwingine inaweza kuwa tofauti hasa pale unapotaka kuanzisha biashara unaweza ukaanza hata kama hauna pesa au una mtaji mdogo.




Yafuatayo ni mambo manne unapaswa kuyazingatia.

**Tunza kidogo kidogo**

Je hauna pesa ya kutosha ili kuanzisha biashara yako, kuwa na subira. Njia rahisi ni kutunza pesa kidogo kidogo kila wiki au hata kila mwezi mpaka pale utakapopata pesa ya kutosha kuanzisha biashara, kwa kufanya hivi kutakuepusha kuingia kwenye madeni. Asilimia flani ya faida utakayoipata unaweza kuiongezea kwenye biashara yako ili kuisaidia ikue.

**Angalia fursa zinazokuzunguka**

Kama utaangalia kwa makini utagundua mara nyingi tunazungukwa na fursa kibao zinazoweza kutuingizia kipato cha ziada. Na unaweza kuanza kutunza kiasi hiki cha pesa utakachokipata ili kikusaidie kufungua biashara.

Kitu cha kwanza kabisa unaweza kuwajulisha majirani zako kwamba unatafuta kazi ili kama watapata taarifa kuhusu kazi uwe wa kwanza kuambiwa.

**Tumia ujuzi ulionao**

Je umewahi kufikiria kuhusu kubadilishana ujuzi? Badala ya kuazima pesa au kununua kifaa chako binafsi, Angalia mazingira yanayokuzunguka. Yawezekana yakakuruhusu kubadilishana kitu kati ya muda, ujuzi na hata vifaa. Labda ngoja nikupe mfano; labda unahitaji cherehani ili kushona bidhaa unazohitaji kuziuza, unaweza kuazima cherehani kwa jirani yako na badala yake unaweza kuwaahidi kuwa utawasaidia kazi zao pale watakapokuhitaji kufanya hivyo.

Kitu cha kwanza ainisha ujuzi na vifaa unavyovihitaji ili kuanzisha biashara yako kisha omba msaada kwa watu wanaokuzunguka. Utashangazwa na jinsi unavyoweza kufanikiwa kirahisi pasipo kuhitaji pesa. Usiogope kuulizalabda wanaweza kukataa ila sio mara nyingi na siku zote watafurahia kukusaidia.

**Tangaza biashara yako mdomo**

Wanafamilia na hata marafiki zako ni njia nzuri sana ya kutangaza biashara yako. Waombe marafiki zako wawaambie marafiki na jamaa zao kuhusu biashara au huduma unazozitoa au hata wanaweza kukusaidia kutangaza kupitia mitandao yao ya kijamii.

Mapendekezo binafsi kutoka kwa watu na pale wanapoizungumzia biashara yako vizuri itaisaidia mno kukua na kukuza jina lako na baada ya muda utashangazwa na jinsi taarifa zinavyosambaa haraka kwa njia ya kuambizana.

Kumbuka, sio lazima kuwa na pesa nyingi ndipo uanzishe biashara. Kuwa mbunifu, tazama fursa zinazokuzunguka,na tumia ujuzi na rasilimali walizonazo watu wanaokuzunguka ili kuanzisha biashara.

Omba msaada kutoka kwa wanafamilia na marafiki ili wakusaidie kutangaza biashara yako nakwambia utashangaa jinsi utakavyofanikiwa pasipo kuhitaji pesa.



# Ya kuzingatia unapoanzisha kilimo biashara

NA MWANDISHI MAALUM

**MKULIMA ni mfanyabiashara, na mfanyabiashara yeyote analenga faida kubwa au hasara kidogo sana. Ni muhimu kwa mkulima kujua thamani ya mazao yake ili aweze kujua ni bei gani anayotakiwa kuuzia mazao yake lakini pia ajue bei ambayo akiuza kwayo itamletea hasara.**

Unapoanzisha mradi wa kilimo biashara, unatarajia mwisho wa siku umalizike kwa kupata faida. Kuna mambo mawili makubwa miongoni mwa mambo kadha wa kadha unayotakiwa kuyajua kabla hujaanza mradi wowote wa kilimo. Mambo hayo ni;

**Mpango mkuu wa kilimo**

Katika kilimo biashara, hili ni jambo la kwanza na muhimu kulifahamu. Farming master-plan ni muongozo wa shughuli zote unazotakiwa kuzifanya katika kilimo tangu kuandaa shamba mpaka kuvuna.

Hatua hii ijumuishe shughuli kama kupanda, kudhibiti magugu, uwekaji wa mbolea na kudhibiti wadudu na magonjwa.

Kwa mfano uwekaji wa mbolea: wakati gani uweke? kiasi gani? uwekeje? Unatakiwa ufahamu haya yote kabla hujaanza mradi wa kilimo ili usipate usumbufu wakati wa utekelezaji.

**Makadirio ya gharama**

Hili ni jambo muhimu sana. Unapofanya kilimo biashara hujaamua kulima ili ujifurahishe tu, unalima ili upate faida. Kwa mantiki hiyo unatakiwa ujue mradi wako utakugharimu kiasi gani katika utekelezaji wake na mwisho wa siku utakulipa kiasi gani?

**Tunza kumbukumbu**

Mali bila daftari hupotea bila habari. Mkulima unatakiwa uwe na daftari la kutunzia kumbukumbu za shughuli zote za shamba. Tunza kumbukumbu za gharama zote ulizozitumia katika kilimo chako.

Mfano; Kama ulikodi shamba au ulinunua, ulilima kwa trekta, ukaajiri watu wa kupanda, ukanunua pembejeo na kama uliajiri watu katika hatua tofauti za kilimo n.k gharama zote ulizotumia katika shughuli hizi zihifadhiwe kwani hii ndio dira yako.



Pima mavuno: Kiasi cha mavuno unaweza kukipima kwa idadi ya magunia au matunda, kwa uzito (Kg) au ujazo (lita au debe). Inapendekezwa kupima kwa gunia, au kilo au/na idadi ya matunda kwa sababu ndio vipimo vinavyotumika kuuza bidhaa sokoni.

Tambua thamani ya mazao: Katika hatua hii gawanya jumla ya gharama za uzalishaji kwa kiasi cha mavuno. Lengo ni kujua umegharamia pesa kiasi gani kwa gunia moja au kilo moja au kwa tunda moja lililovuna. Hii ndiyo thamani ya mazao yako.

Ikiwa gharama za uzalishaji ni kubwa basi mazao yako yanathamani kubwa na hivyo basi ili upate faida ni lazima uuze kwa bei kubwa kuliko thamani yake.

**Panga bei ya mazao**

Baada ya kujua thamani ya gunia moja au kilo moja au tunda moja, hatua nyingine ambayo ndio muhimu zaidi ni kupanga bei sahihi yenye faida utakayouzia mazao yako.

Hapa tunahitaji kupanga bei ya mazao kwa kipimo husika yaani bei ya gunia moja au kilo moja au tunda moja. Bei yenye faida kwako ni ile itakayorudisha gharama zote ulizotumia katika uzalishaji wako.

Ikiwa bei uliyopanga kuuza mazao yako ni ndogo kuliko inayotembea sokoni kwa wakati huo unaweza kuuza au kuangalia namna nyingine ya kuongeza faida zaidi. Ukiona bei ya sokoni ni ndogo kuliko ile uliyopanga kuuzia mazao yako, fanya moja kati ya yafuatayo:

Kwa mazao yanayohifadhika basi yahifadhi kwa muda ili kupisha hali mbaya ya soko. Hakikisha kuwa mazao yako yanahifadhika na una miundombinu ya kuhifadhia kwa angalau miezi mitatu hadi sita.

Kumbuka kuwa unapoamua kuhifadhi unaongeza gharama za ulinzi na za kuhifadhi hivyo utakapotaka kuuza itabidi uzitilie maanani gharama hizi. Kwa maana nyingine ni kwamba unaongeza gharama za uzalishaji kwa hiyo utatakiwa kuongeza ile bei ya kuuzia.

Na kwa mazao yasiyohifadhika kama mboga mboga na matunda, epuka hasara na uuze kurudisha gharama. Hii inamaanisha uza mapema kadri uwezavyo, kwani kuchelewesha kuna hasara Zaidi,

**Angalizo**

Katika mradi wowote wa kilimo biashara utakao ufanya jitahidi kupunguza gharama za uzalishaji ili ujiongezee nafasi ya kupata faida kubwa zaidi. Punguza gharama zote zisizo za lazima, lakini usijisahau kiasi cha kuathiri ubora na wingi wa mavuno.

# ‘Dhahabu ya Damu’ inavyoikausha Goma ya DRC





**NINI kinachotukia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)? Dhahabu ya Damu? Kile kinachotukia nchini humo kwa sasa kinamsikitisha kila mmoja, kwani kimewaacha wakazi wa Mashariki mwa nchi hiyo katika hali tete.**

Waasi wanaonekana kukaribia kuudhibiti moja kwa moja mji muhimu wa Goma mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kufuatia ripoti kwamba wameuteka uwanja wake wa ndege.

Serikali ya Congo imesisitiza kuwa bado inaudhibiti huku mapigano katika baadhi ya maeneo ya mji huo yakiendelea. Maghala yenye chakula na vifaa vya matibabu yameporwa, mashirika ya misaada yanasema.

Mapigano kati ya waasi wa M23 na jeshi na washirika wake yamesababisha hospitali kuzidiwa na majeruhi na miili iliyolala mitaani, kulingana na Umoja wa Mataifa.

Kuongezeka kwa hasira kuhusu mashambulizi ya waasi kulisababisha waandamanaji kulenga balozi za kigeni katika mji mkuu, Kinshasa. Wito wa mazungumzo ya amani kukomesha mapigano unazidi kuongezeka.

Wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wameelezwa jinsi ushindani wa uchimbaji kupita kiasi na biashara ya maliasili huko Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC unavyozidi kuchochea mapigano kwenye eneo hilo, madini kama vile dhahabu na Koltani.

Biashara kutoka eneo la Rubaya linalokadiriwa kuchangia zaidi ya asilimia 15 ya uzalishaji wa madini ya Tantalum, inaipatia M23 dola 300,000 kila mwezi. Hii inatia hofu na lazima ikomeshwe.

Kuna athari nyingi huko na moja ni zitokanazo na janga la kibinadamu hivi sasa Mashariki mwa nchi; Pili, ushiriki wa wanawake kwenye michakato ya kisiasa na amani; na Tatu, umuhimu wa kuchukua hatua mahsusi kulinda raia na wanawake.

Janga la kibinadamu nchini DRC limeathiri vibaya wanawake, wasichana na watoto likiwa viwango vikubwa vya wakimbizi wa ndani, ongezeko la ukosefu wa usalama na uhaba wa chakula.

Zaidi ya hapo ni ongezeko la ukatili wa kingono na kijinsia pamoja na ndoa za lazima kwa watoto wa kike na watoto hao kujikuta wanalazimika kujitumbukiza kwenye biashara ya ngono ili kujikimu kimaisha.

Nchi jirani ya Rwanda imeshutumiwa kwa kuunga mkono kundi la M23 linaloongozwa na Watutsi huku likipiga hatua haraka katika miezi ya hivi karibuni katika eneo hilo lenye utajiri mkubwa wa madini.

Mji wa Goma ulio kando ya ziwa, kwenye mpaka na Rwanda, ni kitovu muhimu cha usafiri na biashara karibu na vyanzo vikubwa vya madini ambayo ni muhimu katika utengenezaji wa simu za mkononi miongoni mwa mambo mengine.

Kufuatia mkutano wa Jumanne, Umoja wa Afrika (AU) ulitoa wito kwa M23 kuweka chini silaha zake.

Kamishna wa amani na usalama wa AU, Bankole Adeoye, alilaani vurugu za M23 na vikosi vingine vyote hasi na anatoa wito wa kuheshimiwa kikamilifu uhuru wa DR Congo, umoja na uadilifu wa eneo.

Wanadiplomasia walipokuwa wakijadili hali hiyo, waasi hao walionekana kupata nguvu huko Goma.

"Wamechukua udhibiti wa uwanja wa ndege, wapiganaji wa M23 wapo," chanzo cha usalama kiliambia shirika la habari la AFP.

"Zaidi ya wanajeshi 1,200 wa Congo wamejisalimisha na wamezuiliwa katika (kambi ya Umoja wa Mataifa) kwenye uwanja wa ndege."

Mapema Jumanne, Adelheid Marschang, mratibu wa dharura wa Shirika la Afya Ulimwenguni kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo alisema kuwepo kwa "mamia ya watu hospitalini, wengi wamelazwa wakiwa na majeraha ya risasi".

Wakizungumza na waandishi wa habari mjini Geneva, Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) imesema hospitali yake mjini Goma imepokea zaidi ya majeruhi 100 katika muda wa saa 24 pekee, idadi ambayo ilipokea awali kwa muda wa mwezi mmoja.

Ilisema kuwa hali hii iliwalazimu wafanyakazi wake kugeuza maegesho ya gari ya hospitali kuwa kitengo cha kufanya tathmini ya awali ya wagonjwa au majeruhi.

Utumiaji wa silaha nzito za kivita katika maeneo yenye watu wengi husababisha majeraha makubwa, haswa miongoni mwa watoto, iliongeza.

Mjini Kinshasa, umati wa watu wenye hasira ulilenga balozi za Ufaransa, Kenya na Uganda miongoni mwa nyingine. Walivamia barabarani, wakichoma magurudumu na kusababisha msongamano wa magari.

Pamoja na vifo vya raia, Afrika Kusini ilisema Jumanne kwamba wanajeshi wake wengine wanne, ambao wako DR Congo kama sehemu ya juhudi za kulinda amani, walikufa kutokana na mapigano na M23.

Hii inafanya jumla ya vifo vya Afrika Kusini kufikia 13. Malawi na Uruguay pia zimepoteza askari wa kulinda amani.

Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa siku ya Jumatatu alizungumza na mwenzake wa Rwanda Paul Kagame, huku wawili hao wakikubaliana kuhusu hitaji la dharura la kusitishwa kwa mapigano na kuanzishwa tena kwa mazungumzo ya amani.

Ilikuja wakati Waziri mpya wa Mambo ya Nje wa Marekani Marco Rubio alipokuwa akilaani shambulizi la M23 katika mazungumzo na Rais wa DR Congo Félix Tshisekedi.

Katika taarifa yake, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema kiongozi huyo wa Congo alikubaliana kuhusu haja ya kuanzisha upya mazungumzo ya amani "haraka iwezekanavyo" na Rwanda.

Rubio pia alizungumza na Rais wa Kenya William Ruto, akikubali kusukuma mbele mazungumzo ya amani. Mkutano ulioitishwa na kiongozi wa Kenya kati ya Tshisekedi na Kagame umepangwa kufanyika Jumatano.

Wakati wa mkutano wa dharura wa Umoja wa Mataifa siku ya Jumapili, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ilidai vikwazo dhidi ya Rwanda, ikisema kuwa vikosi vyake vimevuka mpaka katika eneo lake kwa kile ambacho ni sawa na "tangazo la vita".

Kufuatia mkutano huo, Umoja wa Mataifa ulilaani maendeleo ya M23 na "kupuuzwa kwa wazi kwa uhuru na uadilifu wa eneo la DR Congo", ikiwa ni pamoja na uwepo wa "majeshi ya nje".

Rwanda siku za nyuma ilikanusha uungaji mkono wa moja kwa moja kwa M23, lakini mkuu wa kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa Jean-Pierre Lacroix amesema hakuna shaka kuwa wanajeshi wake walikuwa wakiwaunga mkono waasi.



# Kanuni 12 za kilimo bora chenye tija



NA MWANDISHI MAALUM

**TANZANIA ni moja ya nchi zinazotegemea sana kilimo kama chanzo cha mapato na chakula kwa wananchi wake. Hata hivyo, sekta hii muhimu inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo wakulima wengi kukosa elimu sashihi ya mbinu bora za kilimo, matumizi mabaya ya ardhi na rasilimali za asili, magonjwa na wadudu wa mimea, na changamoto za kiuchumi na kibiashara.**

Hii inamaanisha kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuweka mkazo katika kuboresha kilimo na kuhakikisha kuwa wakulima wanatumia mbinu bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kufikia malengo ya maendeleo ya kilimo na uchumi wa taifa.

Makala hii inalenga kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu kanuni 12 za kilimo bora Tanzania na jinsi zinavyoweza kutumika katika kuongeza uzalishaji wa mazao.

### Kanuni za kilimo bora

Kanuni hizi zinajumuisha Kuandaa shamba mapema, matumizi ya mbegu bora, Kupanda kwa wakati na kwa nafasi, matumizi bora ya maji, matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu, kudhibiti magugu, magonjwa na wadudu wa mazao.

Pia matumizi ya zana bora za kilimo na teknolojia rafiki, utunzaji wa mazingira, kufuata kanuni za usalama na afya, na kufuata kanuni za uchumi.

Makala hii inalenga kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kanuni hizi na jinsi zinavyoweza kusaidia katika kuongeza uzalishaji wa mazao na kuboresha maisha yao na jamii kwa ujumla.

Pia, inasisitiza umuhimu wa kuendelea kubuni na kutekeleza mbinu bora za kilimo ili kukabiliana na changamoto za sasa na za baadaye katika kilimo.

### Kilimo bora ni nini?

Kilimo bora ni njia ya kilimo inayozingatia matumizi sahihi ya rasilimali za kilimo na mbinu bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija. Kilimo bora hulenga kuhakikisha wakulima wanatumia mbinu bora za kilimo kulingana na aina ya udongo, hali ya hewa, na mazingira yao ili kupata mazao bora zaidi na kwa wingi.

### Kanuni za kilimo bora

Kanuni za kilimo bora ni seti ya miongozo au taratibu za kisayansi zilizofanyiwa majaribio kwa muda mrefu na ambazo zimekubalika zitumike katika kuboresha uzalishaji wa mazao.

Kanuni za kilimo bora ni muhimu sana katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija na kusaidia kuboresha maisha ya wakulima na jamii kwa ujumla.

Kanuni hizi huzingatia mambo mbalimbali kama vile matumizi sahihi ya ardhi, utunzaji wa mazingira, matumizi ya mbegu bora, kufuata kanuni za usalama, afya na uchumi, na kadhalika.

Sasa, tuanze kujadili kanuni moja baada ya nyingine.

### Kuchagua Eneo linalofaa

Kuchagua eneo linalofaa na kuliandaa mapema ni jambo la kwanza kabisa kabla ya kuanza mradi wowote wa kilimo. Kanuni hii inakuhimiza mkulima kuchagua maeneo yanayofaa kwa kilimo kulingana na aina ya mazao unayotaka kulima, hali ya hewa, mwinuko wa ardhi, na aina ya udongo.

### Sifa za eneo linalofaa kwa kilimo

Eneo liwe na udongo wenye rutuba na unaoweza kupitisha maji na hewa vizuri.

Eneo liwe na upatikanaji wa maji safi na ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji. Maji yasiwe na chumvi au sumu ambazo zinaweza kuathiri mimea au afya ya watumiaji.

Eneo liwe tambarare au lenye mteremko mdogo ili kurahisisha shughuli za kilimo kama kupanda, palizi, uvunaji na usafirishaji. Eneo lisilo tambarare linaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo au upotevu wa maji.

Eneo liwe linafikika kwa urahisi kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa pembejeo za kilimo, mazao baada ya kuvuna au wanunuzi kufika shambani.

Eneo liwe salama kutokana na wanyama waharibifu, magonjwa, wadudu au wezi ambao watahatarisha uzalishaji na usalama wa mkulima.


### Andaa shamba mapema

Kuandaa shamba mapema kabla ya msimu wa kupanda ni sehemu muhimu ya uzalishaji wa mazao ambayo inaweza kuwa na athari kubwa kwa mafanikio ya msimu wa uzalishaji. Kama mtaalam wa kilimo, nitaelezea umuhimu wa kuandaa shamba na jinsi itakavyokusaidia kupata mavuno mengi na kupunguza hatari ya kupata hasara.

**Itaendelea kesho**



# Bata wanaweza kuondoa njaa katika kaya yako



NA MWANDISHI WETU

**UFUGAJI wa bata ni moja ya shughuli za kilimo cha mifugo ambazo zimeanza kushika kasi kutokana na faida nyingi zinazohusiana na shughuli hii.**

Bata ni ndege wa kufuga ambao wana uwezo mkubwa wa kuhimili hali tofauti za mazingira, huku wakitoa mazao ya kiuchumi kama nyama, mayai, na manyoya.

Pia ufugaji wa bata unahitaji gharama za awali ambazo ni nafuu ukilinganisha na baadhi ya mifugo mingine.

### Umuhimu wa Kufuga Bata

Kufuga bata kunachangia katika: Usalama wa Chakula kwani huzalisha nyama na mayai, ambayo ni vyanzo vya protini bora kwa binadamu. Ufugaji wa bata unaweza kuwa chanzo cha kipato kwa familia kupitia uuzaji wa mazao yao.

Bata husaidia kudhibiti wadudu shambani na pia kutoa mbolea ya asili kwa mimea. Bata wanahitaji nafasi ndogo na chakula cha gharama nafuu, hivyo kuwafanya kuwa bora kwa wafugaji wenye mitaji midogo.

Fahamu bata wana uwezo wa kuishi katika hali tofauti za hewa na maeneo yenye changamoto kama ukame au unyevunyevu mwingi.

Bata wana uwezo wa kupata uzito kwa muda mfupi, hivyo kufaa kwa ufugaji wa kibiashara, pia huzalisha nyama yenye ladha nzuri, mayai yenye virutubisho vingi, na manyoya yanayotumika kwa ajili ya kutengeneza bidhaa kama mito.

Hawa hula vyakula mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabaki ya jikoni, wadudu, na mimea, tofauti na wanyama wengine wa kufuga, bata wanahitaji gharama ndogo ya matunzo.

Bata wanapokula wadudu kama vile nzige na funza, husaidia kudhibiti magonjwa na mazao mashambani, ila kila kitu hakikosi changamoto na tena zipo nyingi tu katika ufugaji wake.

Changamoto zote hizi zinasababishwa na wafugaji wengi kukosa ujuzi wa kutosha kuhusu ufugaji bora wa bata, pia bata wanaweza kushambuliwa na magonjwa kama homa ya ndege ambayo inaweza kuathiri uzalishaji.

Katika baadhi ya maeneo, soko la mazao ya bata linaweza kuwa dogo au halipo kabisa, ila baadhi ya wafugaji wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kufugia bata.

Wafugaji wanapaswa kupewa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji wa bata, kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora kwa ajili ya usimamizi wa magonjwa na lishe.

Pia kuunda ushirika wa wafugaji wa bata ili kuongeza ushawishi wa pamoja kwenye soko, wafugaji wanapaswa kushirikiana na wataalamu wa mifugo ili kuhakikisha bata wanahudumiwa ipasavyo. Bata na mazao yao kama mayai na nyama yanahitajika sana kwenye hoteli, mikahawa, na kaya, mtaji wa awali wa kufuga bata ni mdogo ikilinganishwa na mifugo mingine kama ng'ombe au mbuzi.

Bata wanazaliana kwa haraka, hivyo kuongeza idadi ya ndege wa kufuga kwa muda mfupi. Ufugaji wa bata una faida kwa mazingira, kwa mfano, hutumika kudhibiti magugu na wadudu shambani.

Ufugaji wa bata ni fursa bora ya kiuchumi kwa watu binafsi na jamii. Kwa kuhakikisha lishe bora, usimamizi mzuri, na kushughulikia changamoto zilizopo, wafugaji wanaweza kufaidika na mazao ya bata kwa kiwango kikubwa.

Aidha bata ni ndege rahisi kufuga, wanaoleta faida kubwa, na wanaochangia katika maendeleo ya sekta ya mifugo.

Kufuga bata ni njia endelevu ya kuboresha maisha na kipato cha kaya nyingi hasa maeneo ya vijijini.



# Mbwa siyo ulinzi tu, ni fedha inayobweka

**UKITAKA kujua mbwa anapendwa na wengi tazama hata watoto wadogo wakiwa wanafuga mnyama huyu, hata kwa njia zisizoeleweka. Watatembea naye, watahakikisha wanamfanya awe kiboko kwa kukamata kila kilicho mbele yake.**

Ufugaji wa mbwa, unawakuwa wa ulinzi na ni shughuli muhimu ambayo inachangia katika kuhakikisha usalama wa mali na watu.

Mbwa wana uwezo wa kutoa ulinzi wa karibu na wana sifa za kipekee ambazo zinawafanya kuwa wazuri katika shughuli za ulinzi.

Katika mwongo huu, tutachambua kwa undani kuhusu mbinu bora za ufugaji, faida, changamoto, na njia za kushinda changamoto hizi.

**Kuhusu Mbwa wa Ulinzi**

Mbwa wa ulinzi ni mbwa waliofunzwa kwa ajili ya kutoa ulinzi kwa mali, watu, na maeneo. Aina maarufu za mbwa wa ulinzi ni pamoja na German Shepherd, Rottweiler, Doberman na Belgian Malinois.

Mbwa hawa wana sifa za kipekee kama vile ujasiri, uwezo wa kufikiri haraka, na nguvu.

Ili kufanikisha malengo ya ufugaji wa mbwa wa ulinzi, ni muhimu kuelewa aina mbalimbali za mbwa wa ulinzi:

**German Shepherd**

Mbwa hawa ni maarufu sana kwa ajili ya ulinzi na ni wajasiri. Wana uwezo mzuri wa kufikiri na kujifunza, hivyo wanaweza kufunzwa kwa urahisi. German Shepherds wanaweza kutumika katika shughuli mbalimbali za ulinzi, kama vile kutafuta madawa au kutafuta watu waliopotea.

**Rottweiler**

Rottweilers ni mbwa wenye nguvu na ulinzi mzuri. Wanaweza kuwa wakali lakini pia ni waaminifu kwa familia zao. Ni muhimu kufundisha Rottweilers kwa mbinu sahihi ili wawe na tabia nzuri.

**Doberman**

Dobermans ni mbwa wenye akili na wana uwezo wa kutoa ulinzi mzuri. Wana uwezo wa kubeba mzigo mzito wa kazi na wanahitaji mafunzo ya kina ili waweze kutimiza majukumu yao ipasavyo.

**Belgian Malinois**

Mbwa hawa ni maarufu kwa kazi ya shughuli za ulinzi wa kitaalamu, kama vile katika polisi na jeshi. Wana nguvu, ujasiri, na uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu bila kuchoka.

**Mbinu Bora za Ufugaji**

Ili kufanikisha malengo ya ufugaji wa mbwa wa ulinzi, wafugaji wanapaswa kufuata mbinu bora za ufugaji: Banda la mbwa ni sehemu muhimu kwa ajili ya ustawi wa mbwa.

Wafugaji wanapaswa kujenga banda lenye nafasi ya Kutosha:, kila mbwa anahitaji angalau mita za mraba 5-10. Banda linapaswa kuwa na nafasi ya kutosha kwa mbwa kuhamahama na kupumzika.

Uingizaji hewa mzuri ni muhimu ili kuzuia matatizo ya kupumua na kuboresha afya ya mbwa. Banda linapaswa kuwa na madirisha ya kutosha ili kuruhusu hewa safi kuingia.

Usafi wa banda ni muhimu ili kuzuia kuenea kwa magonjwa. Hakikisha unafanya usafi wa mara kwa mara kwa kuondoa mavi na uchafu.

Lishe ni msingi wa afya na nguvu za mbwa wa ulinzi. Wafugaji wanapaswa kutoa chakula chenye virutubisho vya kutosha kwa mbwa:

Tumia chakula maalum cha mbwa wa ulinzi kinachokuwa na protini ya kutosha. Chakula hiki kinapaswa kuwa na viambato muhimu kama vile omega-3 na omega-6 kwa ajili ya afya ya ngozi na fur.

Hakikisha mbwa wanapata maji safi kila wakati, kwani maji ni muhimu kwa afya na nguvu zao. Kila mbwa anahitaji angalau lita 3-5 za maji kwa siku.

Huduma bora za afya ni muhimu ili kuzuia magonjwa na kuhakikisha mbwa wanabaki na afya nzuri. Kutoa chanjo dhidi ya magonjwa kama vile parvovirus, distemper, na hepatitis. Chanjo hizi zinasaidia kuzuia magonjwa hatari yanayoweza kuathiri afya ya mbwa.

Fuatilia afya ya mbwa kila siku kwa kuangalia dalili za magonjwa kama vile kikohozi, homa, au upotevu wa hamu ya kula. Endapo mbwa wanapata matatizo ya kiafya, ni muhimu kuwapeleka kwa daktari wa mifugo mara moja.

Tumiza dawa za kuzuia vimelea kama minyoo na kupe. Wafugaji wanapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini uwepo wa vimelea.

Hakikisha banda na mazingira ya mbwa yanakuwa safi ili kuzuia magonjwa. Fanya usafi wa mara kwa mara na tumia dawa za kuua wadudu.

Faida za Ufugaji wa Mbwa

Ufugaji wa mbwa wa ulinzi unakuja na faida kadhaa, ikiwa ni pamoja na ulinzi bora wa karibu kwa mali na watu.

Wanajulikana kwa uwezo wao wa kutambua hatari na kutoa tahadhari mapema. Mbwa wa ulinzi si tu walinzi bali pia ni wanachama wa familia.

Wanajenga uhusiano mzuri na wanachama wa familia na wanaweza kuwa marafiki wa karibu. Ufugaji wa mbwa wa ulinzi unachangia katika kuongeza ajira na kuboresha hali ya maisha ya wafugaji.

Hii ni fursa nzuri kwa vijana na wanawake kujihusisha na shughuli za ufugaji. Mbwa wa ulinzi wanachangia katika kuongeza usalama katika jamii.

Mbwa wa ulinzi wanaweza pia kutumika katika shughuli mbalimbali za kibinadamu, kama vile kutafuta watu waliopotea na kusaidia katika shughuli za uokoaji.

Ingawa ufugaji wa mbwa wa ulinzi una faida nyingi, kuna changamoto kadhaa, magonjwa yanaweza kuathiri afya na uwezo wa kazi wa mbwa.

Gharama za chakula zinaweza kuathiri faida ya mfugaji. Bei ya chakula inaweza kuathiriwa na hali ya hewa na uzalishaji wa mazao.

Wafugaji wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu mbinu bora za ufugaji, jambo ambalo linaweza kuathiri uzalishaji na afya ya mbwa. Mbwa wa ulinzi wanahitaji mafunzo ya kina ili kuzuia tabia zisizofaa kama vile ukali.

Wafugaji wanapaswa kuwa na maarifa ya kutosha katika kufundisha mbwa.

Itaendelea toleo la kesho



# Walipambana wakawa matajiri

**KWA mujibu wa jarida la Forbes, utajiri wa mabilionea kutoka bara hili uliongezeka kwa asilimia 12 zaidi ya mwaka mmoja uliopita. Hivyo hapa tunaangazia vyanzo vya mali walionao na utajiri wao kwa jumla kwa mujibu wa Forbes.**

**Aliko Dangote**

Mtu tajiri barani Afrika ndiye mwanzilishi wa kampuni ya saruji ya Dangote, ambayo ndio kubwa zaidi barani Afrika. Anamiliki asilimia 85 ya hisa za kampuni hiyo.

Kampuni ya saruji ya Dangote huzalisha tani milioni 45.6 kila mwaka na inaendeleza opereshieni zake katika mataifa 10 barani Afrika. Dangote pia anamiliki hisa katika biashara ya chumvi na sukari. Kampuni ya kusafisha mafuta ya Dangote imekuwa ikijengwa tangu 2016 na inatarajiwa kuwa miongoni mwa kampuni kubwa za kusafisha mafuta duniani.

**Nassef Sawiris**

Ni mwekezaji anayetoka katika familia tajiri nchini Misri. Mali yake kubwa ni asilimia 6 ya hisa za kampuni ya kutengeneza sare za michezo ya Adidas. Mnamo mwezi Disemba 2020, alifanikiwa kumiliki asilimia 5 ya hisa za kampuni hiyo iliyoorodheshwa katika soko la hisa la New York.

Kampuni yake ya Madison Square Garden Sports, inamiliki timu ya mpira wa vikapu ya Knicks na NHL Rangers. Anasimamia Kampuni ya OCI, mojawapo ya wazalishaji wakuu wa mbolea, ikiwa na kampuni katika majimbo ya Texas na Iowa.

Kampuni zake zina hisa katika kampuni kubwa ya saruji ya Lafarge Holcim na Adiddas. Ni mmoja wa watu walio katika bodi ya kuisimamia Adidas.

**Oppenheimer**

Akiwa mrithi wa mali ya familia yake, aliuza asilimia 40 ya hisa za kampuni ya almasi ya DeBeers kwa kampuni ya Anglo American kwa Dola bilioni 5.1 mwaka 2012.

Ni mmoja wa watu wa kizazi cha tatu cha familia hiyo kusimamia kampuni ya DeBeers na kuifanya kuwa ya kibinafsi 2001. Kwa miaka 85 hadi 2012, familia ya Oppenheimer ilijipatia sifa kubwa katika biashara ya almasi duniani.

Mwaka 2014, Oppenheimer ilianza kufanya kazi katika kampuni ya Fireblade Aviation mjini Johannesburg, ambayo ilikuwa inaendesha ndege za kubeba abiria ikiwa na ndege 3 na helikopta 2. Anamiliki maili 720 mraba za ardhi ya uhifadhi nchini Afrika Kusini, Botswana na Zimbabwe.

**Johann Rupert**

Ni bosi wa Kampuni ya kubeba mizigo ya Compagnie Financiere Richemont ya Uswisi. Kampuni hiyo inajulikana kwa chapa ya Cartier na Mont blanc.




Ilianzishwa mwaka 1998 kupitia mali kadhaa zilizokuwa zikimilikiwa na kampuni ya Rembrandt Group Limited, ambayo babake aliianzisha miaka ya 1940.

Anamiliki asilimia 7 ya hisa za kampuni ya uwekezaji ya Remgro, ambayo yeye ndiye mwenyekiti pamoja na asilimia 25 za hisa za Reinet kampuni ya uwekezaji iliyo na makao yake makuu mjini Luxembourg.

**Adenuga**

Mtu wa pili kwa utajiri nchini Nigeria alijitengezea utajiri wake kupitia sekta ya mawasiliano ya simu ya Telecom na uzalishaji wa mafuta. Kampuni yake ya simu Globacom ndiyo ya tatu kwa ukubwa nchini Nigeria ikiwa na wateja milioni 55.

Kampuni yake ya uchimbaji mafuta ya Conoil Producing inafanya opereshieni katika visima sita vya mafuta katika eneo la Niger Delta.

Adenuga anamiliki shahada ya uzamili ya usimamizi wa Biashara katika Chuo Kikuu cha Pace mjini New York, akijisomesha mwenyewe wakati akifanya kazi kama dereva wa teksi. Alijipatia milioni yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 26 wakati alipokuwa akiuza vinywaji baridi.

**Abdulsamad Rabiu**

Ndiye mwanzilishi wa Kundi la Kampuni za BUA, msururu wa kampuni zinazozalisha saruji, sukari na ujenzi na uuzaji wa nyumba.

Mapema mwezi Januari 2020, Rabiu aliunganisha kampuni yake ya kibinafsi ya Obu Cement na kampuni iliyoorodheshwa katika soko la hisa ya Cement Co kutoka kaskazini mwa Nigeria ambayo aliidhibiti.

Uunganishaji wa kampuni hizo mbili ulizalisha kampuni ya BUA Cement Plc ambayo inafanya biashara ya hisa katika soko la hisa la Nigeria ambapo Rabiu anamiliki asilimia 98.5 za hisa zake. Rabiu, mwana wa mfanyabiashara, alirithi ardhi kutoka kwa babake. Alianzisha biashara yake mwenyewe 1988 akinunua kutoka nje mabati, chuma na kemikali.

**Issad Rebrab ana thamani ya $4.8b**

Ndiye mwanzilishi afisa mkuu mtendaji wa kampuni ya Cevital, kampuni kubwa nchini Algeria. Cevital inamiliki kampuni kubwa ya sukari duniani ikiwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni 2 za sukari kila mwaka.

Cevital pia inamiliki makampuni ya Ulaya ikiwemo kundi la kampuni za kuuza vitu vya nyumbani Brandt, kampuni moja ya kutengeneza vyuma nchini Italia na kampuni nyengine ya kusafisha maji ya Ujerumani.

**Naguib Sawiris**

Anatoka katika familia tajiri nchini Misri. Ndugu yake Nassef pia ni bilionea. Alijipatia utajiri wake katika mawasiliano ya simu kwa kuuza kampuni ya Orascom Telecom mwaka 2011 kwa kampuni ya mawasiliano ya simu nchini Urusi, VimpelCom (sasa ikijulikana kama Veon) katika mazuo yalioshirikisha mabilioni ya dola.

Ni Mwenyekiti wa kampuni ya uwekezaji ya Orascom TMT, ambayo ina hisa na mali nchini Misri pamoja na kumiliki kampuni ya Intaneti nchini Italia. Kupitia kampuni yake ya Media Globe Holdings, Sawiris anamiliki asilimia 88 ya huduma ya televisheni ya malipo na kampuni ya habari ya Euronews. Pia alitengeneza eneo la kifahari la burudani la Silversands katika kisiwa cha Caribbean cha Grenada.

**Patrice Motsepe**

Ni mwanzilishi na mwenyekiti wa kampuni ya African Rainbow Minerals, ambapo alikuwa bilionea mwaka 2008 - akiwa Mwafrika wa kwanza kuorodheshwa katika orodha ya jarida la Forbes. Mwaka 2016.

Alizindua kampuni ya kibinafsi African Rainbow Capital ilioangazia uwekezaji barani Afrika. Motsepe pia anamiliki hisa katika kampuni ya Samlam, kampuni ya huduma za fedha iliooridheshwa katika soko la hisa na ni rais na mmiliki wa klabu ya soka ya Mamelodi Sundowns.

Mwaka 1994, alikuwa mwanzilishi mwenza wa kwanza mweusi katika kampuni ya mawakili ya Bowman Gilfillan mjini Johannesburg na baadaye alianzisha biashara ya huduma za kutoa kandarasi za uchimbaji madini. Mwaka 1997, alinunua mashine za uchimbaji madini wa kiwango cha chini na baadaye kuziuza ambapo alijipatia faida kubwa.

**Koos Bekker**

Anasifiwa kwa kubadili kampuni ya kuchapisha magazeti Nasper kuwa mwekezaji wa kibiashara na runinga. Aliiongoza Nasper kuwekeza katika intaneti ya China na kampuni ya habari ya Tencent mwaka 2001 - Huo ndio uwekezaji uliompatia fedha nyingi zaidi.

Mwaka 2019, Nasper iliwekeza mali yake katika kampuni mbili ambazo hisa zake zilikuwa zinauzwa kwa raia, kampuni ya burudani ya Multichoice Group na Prosus ambayo inamiliki hisa za Tencent. Iliuza asilimia 2 ya hisa za Tencent mwezi Machi 2018, kwa mara yake ya kwanza ikipunguza hisa zake, lakini ikasema wakati huohuo kwamba kamwe haitauza hisa hizo kwa kipindi cha miaka mitatu.

**Mohammed Dewji**

Anaongoza Kampuni ya METL, kundi la makampuni yaliyoanzishwa na baba yake mwaka 1970. METL inashiriki utengenezaji wa nguo, unga wa ngano, vinywaji na mafuta ya kupikia katika eneo la mashariki, kusini na katikati mwa Afrika.

METL inafanya opereshieni zake katika mataifa sita ya Afrika na ina mpango wa kupanua opereshieni hizo katika mataifa mengine. Dewji, ambaye ndiye Mtanzania wa pekee Bilionea alitia saini mpango wa Giving Pledge 2016. Akiahidi kuchangisha nusu ya mali yake kwa wahisani.

# Mikel Arteta
# Moja haikai, mbili haikai



LONDON, England

**TANGU alipokabidhiwa benchi la ufundi Desemba 31, mwaka huu, kocha wa Arsenal raia wa Hispania, Mikel Arteta, amesajili wachezaji 31.**

Je, ni wapi alipofaulu katika usajili huo? Ni wapi alipofeli? Makala haya yanachambua baadhi tu ya wachezaji hao 31. Endelea...

**WILLIAN**

Kiungo huyo wa kimataifa wa Brazil alitua Arsenal akiwa mchezaji huru. Usajili huo ulikuja baada ya Willian kufanya vizuri msimu wa 2019-20 akiwa na wakali wa Stamford Bridge, Chelsea.

Wakati anasaini mkataba wa miaka mitatu, mchezaji huyo alisema Mikel Arteta amemchukua ili kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, baada tu ya kucheza mechi moja kiwango cha juu katika mchezo wa kwanza dhidi ya Fulham, ambapo aliweka 'asisti' mbili, mambo yakaanza kwenda hovyo kwa nyota huyo. Alivunjiwa mkataba akiwa amecheza msimu mmoja tu Emirates.

**RUNAR ALEX RUNARSSON**

Baada ya Emiliano Martinez kuondoka, Arteta aliamua kumsajili kipa huyo wa kimataifa wa Iceland mwaka 2020. Usajili huo ulilenga kumsaidia kazi kipa namba moja wa wakati huo, Bernd Leno.

Arteta aliwashangaza wengi baada ya kumpa nafasi katika mechi yao ya robo fainali ya Kombe la Ligi dhidi ya Manchester City, ambapo walifungwa mabao 4-1, huku kipa huyo akihusika katika kichapo hicho kutokana na uzembe wake.

**AUSTON TRUSTY**

Arteta walimsajili Januari, 2022, lakini aliishia kutolewa kwa mkopo Birmingham, kabla ya kupigwa Sheffield United. Ni kwa maana hiyo, aliondoka akiwa hajacheza hata mechi moja pale Emirates.

NUNO TAVARES

Aliposajiliwa mwaka 2021 kwa dau dogo tu la Pauni milioni nane, Arteta alisema: "Ni mmoja ya wachezaji wanaokuja vizuri." Kinyume cha matarajio, Tavares hajaweza kuwa mchezaji wa kutegemewa Emirates.

**CEDRIC SOARES**

Ni usajili wa kwanza wa Arteta. Arsenal waliochukua kwa mkopo kutoka Southampton lakini majeraha yalimfanya abaki nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Cha kushangaza, licha ya kutokuwa na msaada kikosini, bado mabosi wa Arsenal walimpa mkataba wa miaka minne mwaka 2020. Kwa kushindwa kung'ara, Arsenal waliamua kumuuza Southampton kwa kitita cha Pauni milioni 25.

**GABRIEL JESUS**

Mwaka 2022, Arsenal walimng'oa Manchester City kwa kitita cha Pauni milioni 45. Ni usajili uliotabiriwa kuibeba Arsenal, hasa kutokana na uwezo na uzoefu mkubwa alionao nyota huyo wa Kibrazil.

Hata hivyo, mambo hayajaenda sawa kwa Jesus. Changamoto kubwa inayomkabili nyota huyo ni wimbi la majeraha.

**JURIEN TIMBER**

Mholanzi huyo alisajiliwa na Arsenal mwaka 2023, ambapo Washika Bunduki hao waliweka mezani kitita cha Pauni milioni 38.

Timber aliyesajiliwa baada ya kiwango bora alichokuwa nacho katika kikosi cha Ajax, ni mchezaji muhimu kwa Arsenal katika msimu wake wa pili klabuni hapo.

**KAI HAVERTZ**

Wengi waliponda usajili huo. Arsenal ilitumia Pauni milioni 65 kumng'oa katika kikosi cha Chelsea. Kwa sasa, Havertz ndiye tegemeo la safu ya ushambuliaji ya Arsenal, licha ya udhaifu wake wa kukosa mabao ya wazi.

**JORGINHO**

Ni usajili uliopongezwa na wengi. Mosi, ulilenga kuwadhohofisha wapinzani, Chelsea. Pili, ni usajili wa mchezaji bora na mwenye uzoefu mkubwa si tu wa Ligi Kuu ya England, bali pia soka la Ulaya kwa ujumla. Kwa sasa, Jorginho ni mchezaji muhimu katika safu ya kiungo wa Arsenal.

**LEANDRO TROSSARD**

Arsenal walilenga kumsajili Mykhailo Mudryk mwaka 2023 lakini walipigwa bao na Chelsea. Ni baada ya kumkosa, ndipo walipomgeukia Trossard aliyekuwa akiwika katika eneo la kiungo la Brighton.

Trossard ni mchezaji muhimu kwa Arsenal, ambapo ameshaingia kambani mara 23 na kutoa 'asisti' 17 katika mechi 99 alizoshuka dimbani. Ni usajili ulioigharimu Arsenal kiasi cha Pauni milioni 27 tu.

**BEN WHITE**

Usajili wa bei mbaya ulioigharimu Arsenal kitita cha Pauni millioni 50. Si tu eneo la kati, bali pia White amekuwa akitumika kucheza eneo la mlinzi wa kulia katika kikosi cha Washika Bunduki wa London

**DAVID RAYA**

Ujio wake ulihitimisha nafasi ya Ramsdale kuanza katika kikosi cha Arsenal. Arteta alimsajili kwa mkopo, kabla ya kumchukua moja kwa moja kutoka Brentford, usajili huo ukigharimu kitita cha Pauni milioni 27.

Raya aliumaliza vizuri msimu uliopita na sasa ndiye chaguo la kwanza la Arteta katika lango la Washika Bunduki.

**GABRIEL MAGALHAES**

Arsenal waliinasa saini yake kwa ada ya Pauni milioni 27. Ukweli ni kwamba si pesa ndefu Kwa kiwango bora kinachooneshwa na beki huyo wa kimataifa wa Brazil.

Uwezo wake wa kucheza mipira ya juu, si tu umekuwa msaada mkubwa kwenye ulinzi, bali pia Magalhaes huutumia kuifungia Arsenal mabao ya vichwa.

**DECLAN RICE**

Kwa pesa ndefu waliyotumia Arsenal kumsajili, wengi waliitaja kuwa 'biashara kichaa'. Hata hivyo, kwa sasa nyota huyo wa zamani wa West Ham United ndiye muhimili wa safu ya kiungo ya Arsenal.

**MARTIN ODEGAARD**

Arsenal walianza kwa kumsajili kwa mkopo, kabla ya kulipa Pauni milioni 30 ili kumsajili moja kwa moja. Tangu hapo, Odegaard amekuwa mchezaji muhimu kwenye eneo la kiungo.

Si tu ndiye nahodha wa kikosi, bali pia ameshafunga mabao 36 na kutoa asisti 31 katika mechi 170 alizocheza akiwa na 'uzi' wa Arsenal.

**MARQUINHOS**

Winga wa Kibrazil aliyeshindwa kung'ara Emirates na sasa anacheza kwa mkopo huko kwao akiitumikia Fluminense. Hii ni mara yake ya tatu kutolewa kwa mkopo baada ya kukwama kujihakikishia namba Emirates.

**Albert Sambi Lokonga**

Ulionekana ni usajili mzuri baada ya Washika Bunduki kulipa Pauni milioni 17 kumsajili nyota huyo kutoka katika klabu ya Anderlecht ya Ligi Kuu ya Ubelgiji. Hii ni mara yake ya tatu kupeleka kwa mkopo na sasa anakipiga Sevilla.

**PABLO MARI**

Arsenal walimsajili mwaka 2020. Ni miezi sita tu baada ya nyota huyo kusajiliwa na Flamengo ya huko Brazil. Baada ya usajili huo wa Pauni milioni 12, Mari aliishia kuwa mchezaji wa akiba pale Arsenal. Ameshauzwa moja kwa moja.

**FABIO VIEIRA**

Wakati wa usajili wa mwaka 2022, Arsenal waliweka mezani ofa yao ya Pauni milioni 30 kumng'oa katika kikosi cha Porto.

Hata hivyo, changamoto ya majeraha ya mara kwa mara ilimzuia mshambuliaji huyo kung'ara Emirates. Kwa sasa, Vieira anacheza kwa mkopo katika klabu yake hiyo ya zamani ya Ligi Kuu ya Ureno.

**RAHEEM STERLING**

Washika Bunduki walimsajili wakati wa dirisha kubwa la mwaka jana. Winga huyo alisajiliwa akitokea Chelsea. Hata hivyo, kwa kipindi chake cha mkopo, Sterling hajaweza kuonesha faida ya usajili wake.

**MATT TURNER**

Baada ya kusajiliwa mwaka 2022, kipa huyo alionesha kiwango kikubwa katika mechi za Kombe la Ligi, ambapo aliweza alicheza mechi nne bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa. Aliondoka Emirates na kutimkia Nottingham Forest.

**MAT RYAN**

Ryan alisajiliwa kwa mkopo akitokea Brighton. Ni kipa aliyesajiliwa kumsaidia kazi Leno baada ya Runarsson kuonekana 'kimeo'.

Shabiki huyo wa Arsenal alionesha kiwango kizuri katika mechi zake tatu za mwanzo lakini Arteta aliamua kumfungulia mlango wa kutokea baada ya kumalizika kwa kipindi chake cha mkopo.



# BUENDIA

## Atazamwa villa




LONDON, England

KIUNGO wa Aston Villa, Emiliano Buendia, ameingia kwenye rada za mabosi wa klabu ya Bayer Leverkusen.

Wajerumani hao wanamtaka kwa mkopo lakini Villa wao wanataka biashara ifanyike moja kwa moja.

## CASADEI KUPIGWA MNADA




**LONDON, England**

**CCHELSEA wamekubali ofa ya euro milioni 12 zilizowekwa mezani na klabu ya Lazio kwa ajili ya kiungo wao, Cesare Casadei.**

**Mkataba huo ni wa mkopo ambapo Lazio wataweza kumsajili moja kwa moja.**

**%%%%%**

## MOURINHO AMUITA FATI



ATHENS, Uturuki

KOCHA wa Fenerbahce ya Uturuki, Jose Mourinho, anamtaka mshambuliaji wa Barcelona raia wa Hispania, Ansu Fati. Mourinho 'Special One' amepanga kumchukua kwa mkopo nyota huyo mwenye miaka 22.

## BENRAHMA KWENDA SAUDIA



RIYADH, Saudia

MSHAMBULIAJI wa Lyon, Said Benrahma, huenda akajiunga na moja ya klabu za Ligi Kuu ya Saudi Arabia.

Kwa mujibu wa ripoti, nyota huyo raia wa Algeria anatakiwa na Neom SC ya Ligi Daraja la Pili.

Mjasiriamali spoti
MJASIRIAMALI JANUARI 30, 2025
Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# YANGA HII HAIPOI!

NA MWANDISHI WETU

**YANGA kwa sasa inapiga hesabu kali za Ligi Kuu Tanzania Bara, huku kikosi kizima kikiapa kitafanya kweli katika michuano hiyo kwani kinataka kuhakikisha inatetea taji lake hilo.**

Hili lipo kwa Kocha wa Yanga, Sead Ramovic kwani anaonekana hesabu zimeanza kuelekea mchezo huo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar ambao unatarajiwa kuchezwa Uwanja wa KMC, Complex, Februari Mosi 2025.

Mchezo uliopita ulikuwa ni wa Kombe la Shirikisho la FA ambapo baada ya dakika 90 ubao ulisoma Yanga 5-0 Copco huku ingizo jipya Israel Mwenda akiandika rekodi ya kutoa pasi mbili kwenye mchezo huo.

Kocha huyo ana tuzo ya kocha bora ndani ya Desemba 2024 baada ya kufanya kazi kubwa kwenye mechi nne mfululizo ambazo Yanga ilishuka uwanjani katika ligi namba nne kwa ubora.

Yanga ilipata ushindi kwenye mchezo dhidi ya Tanzania Prisons ubao wa Uwanja wa KMC Complex uliposoma Yanga 4-0 Tanzania Prisons, Dodoma Jiji 0-4 Yanga, Yanga 3-2 Mashujaa, Yanga 5-0 Fountain Gate mchezo huu ulichezwa Uwanja wa KMC, Complex.

Yanga iliandika rekodi ya kuwa timu ya kwanza Bongo kupata ushindi mkubwa bila kuruhusu bao kwa kuwa timu ya kwanza kupata ushindi mkubwa ilikuwa ni Simba 5-2 Kagera Sugar, mchezo uliochezwa Uwanja wa Kaitaba.

Katika mechi nne, safu ya ushambuliaji ya Yanga ilifunga mabao 16 na safu ya ulinzi ikiruhusu mabao mawili pekee ilikuwa dhidi ya Mashujaa mchezo uliochezwa Uwanja wa KMC, Complex.

Kocha wa Simba, Fadlu Davids naye aliingia fainali ndani ya Desemba ambapo alikamilisha mzunguko wa kwanza akiwa namba moja na pointi 40 kibindoni baada ya kucheza jumla ya mechi 15 kwenye ligi safu ya ushambuliaji imefunga mabao 31 na ukuta umeruhusu mabao 5.

Kocha Rachid Taoussi wa Azam FC ni mechi 16 timu hiyo imecheza ikiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo na pointi zao kibindoni ni 36 safu yao ya ushambuliaji imetupia mabao 25 na ukuta umeruhusu mabao 8.




## Simba yataka CAF 'wawape wabaya' wao

NA ASHA SEKEFU

**WAKATI Simba ikitarajiwa kukutana na timu moja kati ya Stellenbosch ya Afrika Kusini, ASEC Mimosas ya Ivory Coast au Al Masry ya Misri, Kocha Mkuu wa Klabu hiyo, Fadlu Davids, amesema haiogopi timu yoyote ambayo watapangwa kucheza nayo hatua ya Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Aidha, alisema lengo la kutaka kuongoza kundi lilikuwa na nia moja tu ya kuanzia mechi ugenini na kupata faida ya kumalizia nyumbani na si vinginevyo.

Fadlu alisema hayo juzi, baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 6-0 Jumapili iliyopita dhidi ya Kilimanjaro Wonders katia mchezo wa Kombe la Shirikisho la CRDB.

Alisema haiogopi timu yoyote hata zile ambazo zimemaliza nafasi ya kwanza angepambana nazo vizuri tu, lakini alipigania zaidi kushinda ili kuongoza kundi kwa ajili ya kumalizia mechi nyumbani bila kujali ni timu gani atakayocheza nayo.

"Tumepata tulichokitaka, nacho ni kumalizia nyumbani tu na kuanzia ugenini, wala hatujali tutacheza na nani, hata hizo timu zilizomaliza juu ya makundi tungeweza kucheza nazo, na tutacheza nazo kama tukivuka hapa.

"Kwa mimi hapa, michuano ya Kombe la Shirikisho sasa ndiyo inaanza. Tunafahamu kufika robo fainali ni mafanikio, lakini kwetu hatuwezi kushangilia sana. Ni mashabiki tu ndiyo wanaopaswa kushangilia kwa sababu ni rekodi na mafanikio ya klabu, lakini kwangu na wachezaji wangu nimewaambia, wasishangilie sana mashindano yenyewe ndiyo yanaanza sasa tunatakiwa kuhakikisha tunakuwa tayari kwa robo fainali," alisema Fadlu.